BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA JUU YA UWASILISHWAJI WA RIPOTI YA MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR KWA MWAKA 2021

---

**Mheshimiwa Spika;** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa mbingu na ardhi, kwa kutujaalia afya njema na taufiki na kutuwezesha kukutana hapa leo hii kwa ajili ya kuendeleza majukumu yetu muhimu ya kuishauri Serikali pamoja na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika chombo hiki muhimu ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika;** aidha, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya uwasilishwaji wa Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa mwaka *2021*.

**Mheshimiwa Spika;** vilevile, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu, Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, ripoti ambayo inaonesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hii kama Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, nambari *1* ya mwaka *2012*, inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika;** kwa dhati kabisa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa yanayoendelea katika Kamati hii kwa kuonesha ufanisi mkubwa katika kutimiza wajibu wao katika chombo hiki kitukufu

katika nchi yetu ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niwataje Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Machano Othman Said | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | - | Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Mjumbe |
| 6. Mhe: Salma Mussa Bilal | - | Mjumbe |
| 7. Ndg: Ali Alawy Ali | - | Katibu |
| 8. Ndg: Mwanaisha Mohammed Kheir | - | Katibu |
| 9. Ndg: Amina Abeid Hemed | - | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika;** aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Unguja na Pemba kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao bila ya kujali ugumu wa kazi wanazozifanya katika kusimamia haki na wajibu wa wananchi kwenye kulinda na kusimamia uchumi wa Zanzibar, licha ya changamoto mbalimbali zinazojitokeza na kukabiliana nazo ikizingatiwa kwamba suala la kukabiliana na vitendo vya rushwa ni gumu na linaleta kila aina ya changamoto kwa wahusika wanaopinga vitendo hivi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati yangu inapongeza kwa dhati mashirikiano yaliopo baina ya Mamlaka hii na Jeshi la Polisi, Ofisi ya DPP pamoja na raia wema. Hata hivyo, Kamati inaiomba Mamlaka hii kuzidisha mashirikiano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili waweze kubadilishana uzoefu utakaoboresha utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika;** katika kuipitia ripoti hii, Kamati yangu imesikitishwa na kuona ushiriki mdogo wa Mamlaka katika Mikutano na Makongamano ya Kimataifa na Kikanda kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumi Uchumi katika nchi hizi

wanachama wa Jumuiya ya Madola. Kwa msingi huo inaonesha wazi kwamba ZAECA wamekosa kuimarisha mashirikiano yao na Mashirika ya Kimataifa na ya Kikanda pamoja na kukosa msaada wa kitaalamu kupitia Mashirika haya ya nchi wananchama.

**Mheshimiwa Spika;** vilevile, Kamati inaishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa inazidisha juhudi zao za kutoa uelewa kwa wananchi juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi kwani kiuhalisia bado vitendo hivyo vinaendelea kufanyika katika jamii yetu kwa mujibu wa Takwimu zilizotolewa na Mamlaka, tuhuma za makosa ya rushwa na uhujumi uchumi zimeongezeka hadi *223* kwa mwaka *2021* ambapo makosa ya Ubadhirifu wa Mali na Mapato yamechukua nafasi kubwa na kufikia asilimia 48.5 na makosa ya matumizi mabaya ya Ofisi za Umma yanaongoza kwa aslimia 39.5 kwa tuhuma zote zilizoripotiwa.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inataka kufahamu ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya tuhuma za ubadhirifu wa mali na mapato ya Serikali pamoja na matumizi mabaya ya Ofisi kwa wahusika, kwani vitendo hivyo vimekuwa suala la kawaida kwa baadhi ya watendaji na wakuu wa taasisi za umma hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika;** idadi ya kesi zilizofanyiwa uchunguzi ni chache sana na kasi ya tuhuma hizi ni ndogo ukilinganisha uzito wa suala hili katika nchi yetu. Kwa kuwa ZAECA ina jukumu la kufanya uchunguzi juu ya tuhuma zinazohusiana na rushwa na uhujumu uchumi, hivyo, basi utaalamu wa hali ya juu unahitajika katika uchambuzi wa taarifa, tathmini na uwasilishaji wa majalada kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili jalada linapofunguliwa kusiwe na mapungufu yanayopelekea kesi hizo kuondolewa kiurahisi Mahakamani au kushindwa kabisa kwa tuhuma hizo kupelekwa Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaendelea kuipongeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kwa kuanzisha nambari ya mawasiliano ya bure kwa wananchi ili iwe msaada kwa kutoa taarifa za rushwa na uhujumu uchumi. Sambamba na hilo, Mamlaka imeripoti kwamba kwa mwaka 2021 zaidi simu za bure 4,400 zimepokelewa ikiwa hazihusiani kabisa na masuala ya rushwa na uhujumu wa uchumi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imebaini namba hiyo haikutumika kama malengo

yalivyokusudiwa kutokana na idadi kubwa ya simu zilizopokelwa kuwa za mzaha na zenye kuwavunja moyo. Kamati inaiomba Mamlaka kuwafuatilia kwa ukaribu sana watumiaji wa namba hii ya bure (toll free) ambao wanaenda kinyume na utaratibu uliowekwa, kufuatiliwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa makosa kimtandao ilivyo ili kukomesha makosa haya kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika;** vile vile, Kamati imeridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa katika kuokoa fedha za umma na kusababisha kupanda kwa mapato ya baadhi ya Taasisi ambazo zimefuatiliwa na Mamlaka katika ukusanyaji wa mapato na matumizi sahihi ya fedha. Taasisi hizo ni Idara ya Maendeleo ya Mifugo Zanzibar na Shirika la Bandari Zanzibar ambapo awali Mamlaka iliripotiwa kuwa Taasisi hizi zimekuwa na upotevu mkubwa wa fedha na hivyo kurudisha nyuma juhudi za ukusanyaji wa mapato kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** kutokana na juhudi hizo kubwa na za kishujaa, Kamati inaishauri Serikali kuangalia umuhimu wa kutoa pongezi kwa Mamlaka kwa kuwapatia tunzo maalumu au kuwa na utaratibu ambao utawasaidia kupata asilimia ndogo kutoka mali waliyookoa ili kuongeza ari na hamasa katika kujitolea kwa kazi hii ngumu yenye kuhatarisha maisha yao.

**Mheshimiwa Spika;** Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar inafanya kazi kubwa na ngumu katika kuwafikia wananchi na kuwaelimisha juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa nchi yetu. Aidha, juhudi zaidi zinahitajika katika kuwafikia watu wote kupitia makundi mbali mbali katika jamii. Kwa muktadha huo, Kamati inashauri Mamlaka kupitia vilabu vya wanafunzi mashuleni sasa waongeze juhudi zaidi kuwekeza katika vyuo vikuu vya Zanzibar ili elimu hii iwafikie wanafunzi ambao kwa muda mfupi huwa watumishi wa Umma na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imebaini kuwepo changamoto kwa baadhi ya Taasisi ambazo zinafanyakazi na Mamlaka hii kwa kuwatumia bila ya kuzingatia mazingira ya kazi na kibinadamu, hivyo watendaji wa ZAECA huweza kufanya kazi kwa muda mrefu bila ya kupatiwa huduma za chakula na sehemu maalumu za mapumziko, kufanya hivyo ni kinyume na taratibu, miongozo na maadili ya kazi zetu katika kufikia maendeleo endelevu.

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuzifanyia kazi changamoto zinazoikabili ZAECA ambayo ni ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kiuchunguzi, ukosefu wa fedha na uhaba wa wataalamu ili Mamlaka iweze kutekeleza vyema majukumu yake pamoja na kufikia malengo yaliyowekwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2020 -2025 katika kujenga Utawala Bora. Aidha, Kamati inatoa wito kwa wananchi na viongozi kwa ujumla kuwa na utamaduni wa kusajili mali zao ili kuwa na umiliki halali wa mali wanazomiliki.

**Mheshimiwa Spika;** mwisho, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii ya maoni ya Kamati yetu, hivyo naomba waichangie na waunge mkono juhudi hizi ambazo zinafanyika kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika; Naomba Kuwasilisha.**



……………………………………

(Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**